darasahuru.ac.tz

**HALMASHAURI YA WILAYA YA MKALAMA**

**MTIHANI WA KUMALIZA MUHULA WA KWANZA KIDATO CHA KWANZA**

**KISWAHILI**

**MUDA: SAA 2:00** **MEI 2025**

**MAELEKEZO**

i. Mtihani huu una sehemu A na B
ii. Jibu maswali yote
iii. Sehemu A ina alama 15 na sehemu B ina alama 85

**SEHEMU A ALAMA 15**

1. Chagua herufi ya jibu sahihi katika vipengele (i-x) kisha andika herufi ya jibu sahihi katika jedwali.
   i. Neno chachandu lina silabi ngapi? (a). tatu (b) nne (c) tano (d) tisa
   ii. Mwanafunzi hodari anasoma. Neno lililopigiwa mstari ni aina gani ya neno? (a) nomino (b) kielezi (c) kivumishi (d) kiwakilishi
   iii. Ili mawasiliano yawe mazuri wazungumzaji wanatakiwa kutumia (A) lugha ya kiswahili (b) lugha ya taifa (c) lugha fasaha (d) lugha ya asili
   iv. "nimemkuta hayupo", hili ni kosa la; (a) maana (b) mantiki (c) matamshi (d) muundo
   v. tulicheza ngoma na kuimba usiku kucha. katika sentesi hii watenda ni nafsi ipi.(a) ya tatu wingi (b) ya pili (c) ya kwanza (d) ya kwanza wingi
   vi. kila mwandishi huwa na ufundi wake katika utunzi wa kazi za fasihi, je jambo gani ambalo hutofautisha maandishi janeth na mwandishi simba katika utunzi kazi zao. (a) mwandiko (b) mtindo (c) muundo (d) lugha
   vii. dhana gani ya mtu wa kaskazini na nyanda za juu kusini hudokeza utambulisho wa maneno yanayotoka? (a) sauti (b) lafudhi (c) matamshi (d) silabi
   viii. misamiati iliyoingizwa katika kamusi na kukolezwa wino, pia kutoa taarifa ya misamiati hiyo kama vile aina ya neno,asili na namna neno linavyotamkwa. (a) kitomeo (b) kidahizo (c) sampuli (d) kisero
   ix. ni umbo la ndani la kazi ya fasihi ambalo hueleza msanii kwa yale yote aliyokusudia katika kazi yake (a) fani (b) dhamira (c) mtindo (d) maudhui
   x. a,e,i,o,u hizi ni; (a) Irabu (b) silabi (c) konsonati (d) sentensi
2. oanisha dhana zilizopo katika orodha A na maelezo yaliyopo katika orodha B kwa kuchagua herufi ya jibu sahihi.

| **ORODHA A** | **ORODHA B** |
|---|---|
| i. utambulisho wa jamii<br>ii. tafsida<br>iii. utamaduni<br>iv. lugha<br>v. mawasiliano | A. tamathali ya semi inayoficha au kupunguza ukali wa neno.<br>B. Hueleza mambo yatokanayo na utamaduni wa mtanzania<br>C. Upashanaji Habari au taarifa kwa njia ya mazungumzo, maandishi na ishara<br>D. Makubaliano ya Pamoja baina ya wazungumzaji |

| | |
|---|---|
| | E. Mwenendo wa Maisha unaohusisha asili, mil ana desturi na jadi unaotumika katika jamii Fulani<br>F. Hueleza sifa bainifu za jamii Fulani<br>G. Mfumo wa sauti za nasibu unaotumia maneno yanayosemwa na binadamu ambao huwawezesha watu wa jamii Fulani kuwasiliana. |

## SEHEMU B ALAMA 85

3. Eleza umuhimu wa kulinda na kuheshimu utamaduni wa kitanzania.

4. Badilisha nomino zifuatazo kuwa vitenzi.
   i) Wimbo
   ii) Umbo
   iii) Mtoro
   iv) Kilio
   v) Mlo
5. Tunga sentensi zenye miundo ifuatayo kwa kupigia mstari sentensi hiyo kuonesha aina hizo. Mfano; N+T+E=<u>mama</u>/N <u>anapika</u>/T <u>jikoni/E</u>
   **i. H+N+T+E**
   **ii. N+V+V+TS+TS+T**
   **iii. W+t+N+V**
   **iv. W+V+T**
   **v. T**
6. Kama maneno katika kamusi yatapangwa bila kufuata mpangilio maalumu ni changamoto gani zinaweza kujitokeza?
7. Tumia maneno yafuatayo kutunga sentensi kulingana na maana za maneno hayo katika kamusi.
   a) Mgogoro
   b) Kanyaga
   c) Gawa
   d) Chujio
   e) Sabahi
8. Faraja hutumia kamusi kutafuta maana ya misamiati mbalimbali lakini hafahamu kuna taarifa nyingine zitokanazo na kamusi, msaidie kwa kutaja taarifa nne.
9. Bainisha maneno yenye makosa ya kimatamshi katika sentensi zifuatazo kwa kupigia mstari kisha andika sentensi hizo kwa usahihi.
   a) Mwanafunzi anayejitambua hapendagi mzaha katika masomo.
   b) Shule yetu ina vifaa vya samani.
   c) Mti uliokuwa kalibu na bustani ya maua umeanguka.
   d) Mzee kiza amedhuru mbuga za Wanyama.